

TARATIBU ZA KUPATA KIBALI CHA UJENZI

1. KIBALI CHA UJENZI

Kulingana na sheria ya ujenzi wa majengo Mijini si ruhusa kwa mtu yeyote kujenga au kuanza kujenga jengo bila ya:-

- Kutuma maombi kwa mamlaka ya mji.
- Kuwasilisha michoro ya jengo na kumbukumbu husika.
- Kupata kibali kwa maandishi kinachoitwa " Kibali Cha ujenzi".

2. KIBALI CHA AWALI (Plannning consent)

Inashauriwa kupata kibali cha awali kabla ya kuomba kibali cha ujenzi. Hivyo muendelezaji anatakiwa aandae mchoro wa awali (Outline plan) kwa utaratibu unaotakiwa ukionyesha aina ya ujenzi atakaokusudia kufanya ili aweze kupata ridhaa ya kuendelea na hatua za kuandaa michoro ya mwisho.

Faida:

- Kuokoa muda wa gharama iwapo michoro ya mwisho itaonekana kuwa na dosari za kitaalam ambazo zitahitaji kufanyiwa marekebisho.
- Kuwa na uhakika kuhusu mahitaji muhimu ya kuzingatiwa wakati michoro inaandaliwa.

3. JINSI YAKUWASILISHA MAOMBI YA KIBALI CHA UJENZI

Baada ya michoro kukamilika iwasilishwe ikiwa kwenye majalada kwa namna ambayo inaweza kufunguliwa na kusomeka. Michoro hiyo iwasiliswe kwa utaribu ufuatao:-

- Seti tatu za michoro ya jengo (Archectual drawings).
- Seti mbili za michoro ya vyumba (structural drawings) kwa michoro ya ghorofa.

4. MICHORO ILIYOANDALIWA IONYESHE NINI

Michoro itakayoandaliwa inatakiwa ionyeshe mambo yafuatayo:-

- Namna jengo litakavyokuwa (plans sections, elevation, foundation and roof plan).
- Namba na eneo la kiwanja kilipo.
- Jina la mmiliki ardhi inayohusika.

- Jina la mchoraji, ujenzi na anuani.
- Ukubwa wa jengo kwa mita za mraba.
- Ujazo wa kiwanja (Plot coverage).
- Uwiano (Plot ratio).
- Matumizi yanayokusudiwa.
- Idadi ya maegesho yatakayokuwepo.
- Umbali wa jengo kutoka kwenye mipaka ya kiwanja (setbacks).
- Mfumo wa kutoa maji hadi kwenye mashimo.

5. VIAMBATANISHO

- Fomu za maombi zilizojazwa kwa usahihi.
- Hati ya mmiliki wa kiwanja au barua ya toleo.
- Kumbukumbu nyingine zinazohusu kiwanja hicho kama hati za mauzo, makabidhiano n.k.
- Nakala za risiti ya kodi ya kiwanja ya sasa.
- Mabadiliko ya matumizi ya ardhi kama muombaji amebadili matumizi ya awali.

6. HATUA ZINAZOFUATWA KATIKA KUSHUGHULIKIA MAOMBI YA KIBALI

Zifuatazo ni hatua zinazofuatwa wakati wa kuchunguza michoro hiyo:-

- Uhakiki wa miliki.
- Kukaguliwa usanifu wa michoro.
- Kukagua kiwanja kinachokusudiwa kuendelezwa, uchunguzi wa matumizi ya jengo na uwiano.
- Uchunguzi wa maofisa wa afya.
- Uchunguzi wa mipango ya uondoaji maji taka.
- Uchunguzi wa tahadhari za moto.
- Uchunguzi wa uimara wa jengo.
- Kuwasilisha kwenye kikao cha Mipangomiji na Mazingira baada ya kukamilisha taratibu zote.
- Hafimaye kuandika na kutoa kibali.